

NIDHAMU BINAFSI.

- Kwa nidhamu binafsi, chochote kinawezekana. Huu ni ukweli wenye kutia moyo sana kwamba kama una nidhamu binafsi, unaweza kufanya chochote.
- Utatimiza malengo yako kama una nidhamu binafsi. Kinyume chake ni kuwa, kama huna nidhamu binafsi, hutaweza kutimiza malengo. Matokeo yake, utaishia kuhangaika tu na kupoteza muda.
- Utayashinda magumu na changamoto kama utakuwa na nidhamu binafsi. Kama huna, hutaweza kuzing'amua changamoto.
- Ukiwa na nidhamu binafsi, unaweza kujidhibiti, kujitawala na kujiongoza vyema. Hivyo basi, utafanya maamuzi sahihi.
- Nidhamu binafsi huboresha afya zetu na mahusiano yetu.
- Nidhamu binafsi ni nguzo kuu ya mafanikio makubwa ya mtu. Ni kupitia nidhamu binafsi, msingi wa maisha ya mtu unakuwa imara.
- Nidhamu binafsi ni ufunguo wa ajabu unaoweza kufungua milango yote kwa ajili yako na kufanya kila kitu kuwezekana.
- Mtu wa kawaida kabisa anaweza kuinuka na kufika mbali sana kimapanikio iwapo atakuwa na nidhamu binafsi.